DPS NEWCOMER CENTERS (VITUO VYA WAGENI VYA DPS)

MADHUMUNI:
Newcomer Centers (Vituo vya Wageni) ni mipango iliyoko katika shule maalum za DPS vinavyowasaidia wanafunzi wageni nchini Marekani, ambao hawafahamu Kiingereza vyema, wamekatiza masomo yao rasmi katika nchi yao asilia na wamehudhuria shule ya Marekani kwa chini ya mwaka mmoja. Katika Newcomer Centers (Vituo vya Wageni), wanafunzi hujifunza stadi zitakazowasaidia kufanikiwa katika shule za Marekani, pamoja na stadi za msingi za hisababti na kusoma na kuandika Kiingereza. Wanafunzi wengi wageni husalia kwenye mpango wa Newcomer Center (Vituo vya Wageni) kwa muhula mmoja na mihula miwili, hadi wanapokuwa tayari kuhudhuria madarasa katika shule wanayotaka.

MAENEO YA NEWCOMER CENTERS (VITUO VYA WAGENI):

Shule za Msingi	Shule za Kati	Shule za Upili
Isabella Bird Community School 2701 Lima St. Denver, CO 80238 (720) 423-9990 Tovuti ya Shule **Place Bridge Academy (K-5)** 7125 Cherry Creek N. Dr. Denver, CO 80224 (720) 424-0960 Tovuti ya Shule	**Merrill Middle School** 1551 S. Monroe St. Denver, CO 80210 (720) 424-0600 Tovuti ya Shule	**Abraham Lincoln High School** 2285 S. Federal Blvd. Denver, CO 80219 (720) 423-5000 Tovuti ya Shule **DCIS Montbello (6-12)** 5000 Crown Blvd., Denver, CO 80239 (720) 423-5900 Tovuti ya Shule **South High School** 1700 E. Louisiana Ave. Denver, CO 80210 (720) 423-6000 Tovuti ya Shule

KUMTAMBUA MWANAFUNZI WAKO KAMA MGENI:
Wafanyakazi wa ofisini wa shule iliyoko karibu na nyumbani mwako wamefunzwa kushirikiana nawe na familia yako ili kutambua uwekwaji bora zaidi kwa mwanafunzi wako. Huenda ukatumwa kwa Newcomer Center (Kituo kifaacho cha Mgeni) kwa tathmini zaidi ikiwa mwanafunzi wako anatimiza vigezo VYOTE vifuatavyo:

- ❏ Mwanafunzi huyu ana historia ya elimu rasmi kukatizwa au pungufu
- ❏ Alama ya uwekwaji ya W-APT inaashiria kwamba mwanafunzi hafahamu Kiingereza vyema. Ikiwa alama ya W-APT haipo, mwanafunzi huyu anaonyesha ujuzi mdogo wa kusoma na kuandika lugha yake asili na Kiingereza.
- ❏ Mwanafunzi huyu, ameshaandikishwa kuwepo katika shule iliyoko Marekani kwa mihula miwili au chini yake, wakati wa uwekewaji wa kwanza.

DPS ni wilaya iliyochaguliwa, inayomaanisha kwamba una chaguo la kuwaweka wanafunzi wako katika shule iliyoko karibu na nyumbani, ELA Zone School (Shule ya Zoni ya ELA), Newcomer Center (Kituo cha Wageni), au kushiriki katika mchakato wa School Choice (Kuchagua Shule) ili kumwandikisha mwanao awe katika shule yoyote ya DPS. Shule ya DPS iliyoko karibu na nyumbani mwako na ELA Zone Schools (Shule za Zoni ya ELA) huenda zisimkatae mwanafunzi wako kwa sabbau ya uwezo wa lugha.

USAFIRISHAJI:

Wanafunzi wa Shule ya Msingi: Usafirishaji unatolewa kwa Newcomer Center (Kituo cha Wageni) ikiwa wanafunzi wanaishi zaidi ya maili moja kutoka kwa Newcomer Center (Kituo hicho cha Wageni).

Wanafunzi wa Shule ya Kati: Usafirishaji unatolewa kwa Newcomer Center (Kituo cha Wageni) ikiwa wanafunzi wanaishi zaidi ya maili 2.5 kutoka kwa Newcomer Center (Kituo hicho cha Wageni).

Wanafunzi wa Shule ya Upili: Pasi ya basi la umma hutolewa kwa wanafunzi kupitia RTD kwa wanafunzi wanaoishi maili 3.5 kutoka kwa Newcomer Center ((Kituo hicho cha Wageni).

JE, NEWCOMER CENTER (KITUO CHA WAGENI) KINAMFAA MWANAFUNZI WANGU?

Newcomer Centers (Vituo vya Wageni) vinaweza kuwa pahali pazuri kabisa pa wanafunzi kujifunza kuhusu nchi yao mpya, lugha yao mpya na shule yao mpya; lakini familia zinapaswa kuzingatia baadhi ya mambo fulani wanapofikiri kuhusu shule ambayo wanataka mwanao ahudhurie.

Chaguo la Wazazi na Mwanafunzi: Huenda ukawa mgeni kwa mchakato wa uandikishaji katika DPS. Kama wilaya iliyochaguliwa tu, wanafunzi wote na wazazi wao katika DPS wana haki ya kuhudhuria shule *yoyote*, inayomaanisha kwamba kila shule katika DPS iko tayari kutumikia wanafunzi *wote*, bila kujali kiwango chao cha elimu, lugha, au lugha asili.

Ndugu na Familia: Kuna uwezekano kwamba ungependa kuwaweka ndugu, bin/bintiamu, jamaa wa mbali, majirani, au wandani wengine katika shule moja, na hilo ni SAWA. Kwa vile tu mwanafunzi wako amehitimu kwa Newcomer Center fulani (Kituo cha Wageni), haimaanishi kwamba lazima wahudhurie shule hiyo. Shule zinapaswa kuheshimu chaguo lako la uwekwaji.

Usafirishaji:

Wanafunzi wa Shule ya Msingi: Ikiwa wanafunzi hawaishi karibu na stendi ya basi, huenda wakahitajika kutembea masafa marefu hadi kwa iliyoko karibu. Isitoshe, kupelekwa kwa Newcomer Center (Kituo cha Wageni) kwa basi kunaweza kumaanisha kwamba mwanafunzi wako ako kwenye basi kwa saa moja asubuhi na kwa saa moja jioni, jambo linalopaswa kuzingatiwa unapoamua uwekwaji katika Newcomer Center (Kituo cha Wageni).

Wanafunzi wa Shule ya Upili: Kwa vile wanafunzi wakubwa hupokea pasi ya basi la umma, huku kunaweza kumaanisha kwamba wanafunzi wanatembea hadi kwenye stendi za basi saa za asubuhi na mapema kabla ya mchana, na saa za usiku kabisa baada ya machweo, na pia kunaweza kujumuisha kusafirishwa hapa na pale wanafunzi wanaposafiri jijini.

NINI KINACHOFUATA?

Ikiwa mwanafunzi wako ametambuliwa kama anayestahiki kuhudhuria Newcomer Center (Kituo cha Wageni), unaweza kuchagua kumwandikisha kwa kujaza fomu ya usajili ya Newcomer Center (Kituo cha Wageni) na kuirejesha kwa ofisi ya shule. Newcomer Center (Kituo cha Wageni) kitawasiliana nawe ili kukupa taarifa zaidi kuhusu unachopaswa kufanya baadaye.

Ukiamua kumwandikisha mwanafunzi wako katika shule yake jirani au katika ELA Zone School (Shule ya Zoni ya ELA) iliyoko karibu, wafanyakazi wa ofisini watakupa nyaraka zinazohitajika ili kukamilisha usajili wao na kuanza kuhudhuria shule.